

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

FURSA YA KUOMBA NAFASI YA UJUMBE KATIKA BARAZA WAKILISHI LA VIJANA LA SHIRIKA LA KIMATAIFA LA MAWASILIANO (ITU GENERATION CONNECT YOUTH ENVOYS)

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutarifu Umma kuwa imepokea fursa kutoka Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU) ya kupendekeza watazania wataokidhi vigezo vya kugombea nafasi ya ujumbe katika Baraza Wakilishi la Vijana la ITU (ITU Generation Connect Youth Envoys). Wagombea wanapaswa kuwa watazania wenye **umri kati ya miaka 18 na 24** ambao wanashauku ya kuwa sehemu ya Baraza tajwa.

Waombaji wanatakiwa kueleza na kutoa ushahidi wa ushiriki wao katika kutumia TEHAMA kwa malengo ya kielimu, maendeleo ya kijamii na uchumi, au uwezeshaji wa vijana. Ushiriki huo unaweza kudhihirishwa kwa njia nyingi, kama vile kupata na kusambaza maarifa, kushiriki katika shughuli za kijamii zinazohusisha TEHAMA, au kubuni, kutengeneza, na kuendesha miradi maalum (pamoja na ile inayoendelea na utekelezaji) yenye kuleta tija katika kijamii, kitaifa, kikanda, au kimataifa.

Kwa mwombaji anaependa kushiriki kwenye fursa hii, tafadhali wasilisha maombi yako TCRA kupitia anwani ya baruapepe ya generationconnect@tcra.go.tz kabla au ifikapo **Jumatatu, 27 Aprili, 2026**. Aidha, kulingana na vigezo tajwa hapo juu, waombaji wanne (4) watachaguliwa na TCRA na kupendekezwa ITU ili washiriki kuomba nafasi ya ujumbe moja kwa moja kwa Baraza Wakilishi la Vijana la ITU kabla ya **Alhamisi, 30 Aprili, 2026**.

TCRA inawahimiza wadau wote, ikiwemo wanachama wa vilabu vya kidijiti, sekta binafsi, vyuo vikuu, vituo vya uvumbuzi na taasisi za Umma, kuwahamisisha vijana wanaokidhi vigezo kuomba nafasi hii.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na TCRA kupitia namba **0800008272** au baruapepe dawatilahuduma@tcra.go.tz.

Imetolewa tarehe **17 Aprili, 2026**.

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.

Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10

Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz